**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS,**

**MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

# TAARIFA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA WATUMISHI WA UMMA KUHUSU UZINDUZI WA MFUMO WA KIELEKRONIKI WA TATHMINI YA HALI YA WATUMISHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Ofisi ya Rais,
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora,
Mtaa wa Utumishi,
Mji wa Serikali Mtumba,
S. L. P 670,
**DODOMA.**

**MACHI, 2022**

**TAARIFA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA WATUMISHI WA UMMA KUHUSU UZINDUZI WA MFUMO WA KIELEKRONIKI WA TATHMINI YA HALI YA WATUMISHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

***Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema, aliyetuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Ninawashukuru wote waliohusika katika kuandaa tukio hili la kuzindua **Mfumo wa Kieletroniki wa Tathmini ya Hali ya Watumishi wa Umma katika Taasisi za Umma**. Mfumo huu umesanifiwa na kujengwa kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali ya Watumishi wa Umma kwa idadi, majukumu yao na vituo wanavyofanyia kazi. Aidha, ninawashukuru ndugu zangu Waandishi wa Habari ambao hakika mmekuwa msaada mkubwa sana kwa Ofisi ninayoiongoza na Serikali kwa ujumla linapokuja suala la kuhabarisha na kuelimisha Umma wa Watanzania, nawashukuru sana.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** wote tunajua kuwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina majukumu mengi ya Kisera na kiutendaji yanayotekelezwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali inayolenga kuimarisha usimamizi wa Rasilimaliwatu tangu mtumishi anapoajiriwa mpaka atakapostaafu. Pia tunajua umuhimu wa Rasilimaliwatu katika kuzifanya rasilimali nyingine ziweze kuleta maendeleo nchini. **Nimekuwa nikisisitiza suala hili mara kadhaa kwamba bila kuisimamia vizuri Rasilimaliwatu basi hizo rasilimali nyingine zote tulizonazo haziwezi kutuletea maendeleo tunayokusudia.**

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** niseme mapema na kwa dhati kabisa kuwa wote tunaona juhudi anazozifanya mama yetu **Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwenye Sekta mbalimbali katika kuiletea maendeleo nchi yetu na watu wake. ***Sisi tunaendelea kumsaidia kufanikisha juhudi hizo katika kutekeleza jukumu la kuimarisha usimamizi na utendaji wa Rasilimaliwatu nchini.*** Ili kufikia azma hiyo pamoja na mambo mengine tunasanifu na kujenga mifumo na taratibu mbalimbali zikiwemo za kuwezesha kuwa na Watumishi wa Umma wenye sifa stahiki kwa wakati sahihi.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** bila shaka wote mnakumbuka kuwa mwezi Januari 2022 mara tu baada ya kuteuliwa niliongea nanyi kupitia Waandishi wa Habari juu ya mwelekeo wa Mifumo ya Utendaji Kazi na niliahidi kurudi kwenu na Mfumo wa Kielektroniki utakaotusaidia kufanya tathmini ya hali ya watumishi katika taasisi za Umma. Nafurahi kuwaarifu kuwa siku hiyo imefika ambapo leo Ofisi yangu itazindua **Mfumo huo wa Kielektroniki wa Tathmini ya Hali ya Rasilimaliwatu katika Taasisi za Umma nchini**.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma,** katika kutekeleza majukumu iliyopangiwa, Ofisi yangu itahakikisha inazingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2030; Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Awamu ya Tatu 2021/22 – 2025/26 pamoja na maono ya Rais wa Serikali ya Awamu ya Sita na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan kuhusu Utumishi wa Umma wa kidijtali na unaofanya kazi kwa uadilifu, kwa bidii, unaotenda haki, unaowajibika kwa hiari na unaozingatia uzalendo wa kitaifa**. Ni jukumu letu sisi Viongozi na Watumishi wote wa Umma kuchapa kazi

kwa utalaamu, ubunifu na weledi wa hali ya juu ili kuhakikisha kuwa Dira ya Maendeleo ya Taifa na maono na azma ya Kiongozi Mkuu wa Nchi yetu yanatimia.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** Mfumo wa Kielektroniki wa Tathmini ya Hali ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma umesanifiwa na kujengwa na Wataalamu wetu wa ndani ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Jambo hili ni la kujivunia kwa sababu bila hivyo Serikali ingeweza kuingia gharama kubwa katika kusanifu na kujenga Mfumo kama huo kwa kutumia Wataalamu au Washauri Waelekezi na pengine wa kutoka nje. Niwashukuru wataalamu wetu pamoja na wote waliosimamia mpaka Mfumo huo kukamilika. Ni jukumu letu kutunza, kusimamia na kuulinda Mfumo huu ili uweze kufanya kazi iliyokusudiwa ipasavyo.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** mara baada ya kusanifiwa na kujengwa kwa Mfumo huo, Ofisi ya Rais - UTUMISHI iliupeleka kwa Waajiri wote waliopo kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara katika Utumishi wa Umma (HCMIS) ili kuingiza taarifa na takwimu sahihi kuhusu idadi na mgawanyo wa watumishi kulingana na huduma zinazotolewa na taasisi za Umma. Kwa taasisi zilizo nje ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara katika Utumishi wa Umma (HCMIS) zilipelekewa nyenzo ya kukusanya taarifa ambazo zitaingizwa kwenye Mfumo wa Kielektroniki kwa ajili ya kuchakatwa zaidi.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** Mfumo tunaozindua leo unalenga kutuwezesha kukusanya, kuchakata na kuchambua taarifa za Watumishi kwa njia ya kisayansi ili kubaini mahitaji halisi ya Watumishi katika Wizara na Taasisi za Umma. Zoezi hili litatusaidia katika kutathmini hali halisi ya Watumishi waliopo na wanaohitajika katika

taasisi zote za umma ili kuweza kuwapanga kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kila taasisi. Kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa na taarifa na takwimu sahihi kuhusu watumishi waliopo, mahitaji ya watumishi wanaohitajika katika kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi. Aidha, matarajio ya zoezi hili ni kuweka msawazisho wa Watumishi wa Umma katika taasisi za Umma. Kwa tathmini iliyopo inabainisha kuwa utoshelevu wa mahitaji ya watumishi kwa taasisi za Umma upo kati ya asilimia 52 hadi 90. Hata hivyo, zipo baadhi ya taasisi ambazo zina watumishi wa ziada katika baadhi ya kada.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** zoezi hili lilianza mwezi Januari 2022 na lilitakiwa likamilike katikati ya mwezi Februari, 2022. Hata hivyo, tukiangalia mwenendo wa zoezi hili mpaka leo inaonesha bado Wizara na Taasisi nyingi hazijakamilisha zoezi hili muhimu. Kwa taarifa tulizo nazo mpaka leo kati ya Wizara na Taasisi 427 zilizo kwenye Mfumo wa HCMIS zote zimeshaanza kutumia Mfumo na zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa zoezi hili na zipo kati ya asilimia 13 hadi 97. Aidha, taasisi 41 kati ya taasisi 70 zilizo nje ya Mfumo wa HCMIS zimeshawasilisha taarifa zao na sasa wataalam wanachakata taarifa hizo kwa ajili ya kuziweka kwenye Mfumo. Hata hivyo bado kuna Wizara na Taasisi nyingi hazijatekeleza maelekezo ya Serikali ipasavyo. Hivyo tunaomba viongozi wa taasisi wawajibike ipasavyo ili tuweze kufikia lengo la zoezi hili muhimu litakaloimarisha usimamizi wa Rasilimaliwatu.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma,** Taarifa za kwenye Mfumo nitakaouzindua leo zimebainisha kuwa zipo Taasisi zilizofanya vizuri na ambazo hazijafanya vizuri katika kuingiza taarifa kwenye Mfumo. Kwa mfano, Taasisi 10 bora zilizofanya vizuri ni pamoja na Shule ya Sheria Tanzania (97%); Tume ya Ushindani (97%); Chuo cha Ardhi Morogoro

(97%); Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala (96%); Ofisi ya Rais Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (95%); Sekretariet ya Mkoa wa Iringa (95%); Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (95%); Mamlaka ya Serikali Mtandao (95%); Taasisi ya Utafiti wa Wanyama Pori (95%); na Wakala ya Mafunzo ya Menejimenti ya Elimu (94%).

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma,** vile vile Mfumo umebainisha Taasisi takribani 94 ambazo hazijafanya vizuri katika kuingiza taarifa kwenye Mfumo kwa sababu bado zipo chini ya asilimia 50 ya utekelezaji wa zoezi hili (*Orodha imeambatishwa*). Kwa mfano, wenzetu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa takribani Halmashauri 39 na Mamlaka nyingi za Maji hawajafanya vizuri kwenye zoezi hili.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** Orodha niliyonayo ni mfano tu wa taasisi nyingi ambazo hazijakamilisha zoezi hili muhimu kwa sababu mbalimbali. Ninapenda nichukue fursa hii kusisitiza na kuagiza waajiri wote wawasimamie Wakurugenzi au Wakuu wa Idara/Sehemu zinazosimamia Rasilimaliwatu katika taasisi zao ili wakamilishe zoezi hili **kabla au ifikapo tarehe 31 Machi, 2022**. Taasisi ambazo hazitakamilisha zoezi hili zitakuwa zimekiuka maelekezo ya Serikali na hatua stahiki zitachuliwa.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** Ninapenda kuwaambia kuwa Ofisi yangu pamoja na Serikali kwa ujumla tumejipanga kuhakikisha zoezi hili linafika mwisho ili kufikia lengo lililokusudiwa. Ni imani yangu kuwa, Wakuu wa Taasisi za Umma na watumishi watazingatia maelekezo niliyotoa na yale ambayo yamekuwa yakitolewa kwa ajili ya kulifanya zoezi hili liwe na tija. Kwa kufanya hivyo tutaweza kufikia azma ya Mheshimwa **Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita kuwa na

Utumishi wa Umma wenye uwiano wa watumishi unaouzingatia mahitaji na ujuzi stahiki katika maeneo husika.

**Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma;** Kwa niaba ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo nimepewa dhamana ya kuiongoza ninapenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru **Watumishi Wote wa Umma pamoja na viongozi katika ngazi mbalimbali** kwa namna ambavyo wamekuwa wakijitoa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi. Ni imani yangu kuwa tutaendelea kuboresha namna tunavyofanya kazi ili kuleta tija na matokeo chanya katika maeneo yetu ya kazi.

***Ndugu Viongozi na Watumishi wa Umma,*** baada ya kusema haya na kwa vile nilikuwa sijazindua Mfumo huu, sasa nipo tayari kuzindua rasmi **Mfumo wa Kielektroniki wa Tathmini ya Hali ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma** na ninapenda niwaoneshe ***muonekano wa Mfumo*** huo.

***ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA***

***KAZI IENDELEE............***